# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU**

**MAREKEBISHO YA ORODHA YA MAENEO YA UCHAGUZI KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025, KUTENGUA UTEUZI WA WAGOMBEA KATIKA MAENEO YA UCHAGUZI YALIYOFUTWA, KUFUTWA KWA VITUO VYA KUPIGIA KURA 292 VILIVYOPO KATIKA KATA ZILIZOFUTWA NA KUANZISHA VITUO 292 KWENYE KATA WALIPOHAMISHIWA WAPIGA KURA HUSIKA**

*Ndugu Wananchi,*

Kupitia Tangazo la Serikali Na. 596 la tarehe 03 Oktoba, 2025 Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliyatangaza maeneo ya Ulyankulu Wilaya ya Kaliua Mkoa wa Tabora, Katumba Wilaya ya Mpanda Mkoa wa Katavi na Mishamo Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi kuwa maeneo tengefu kwa ajili ya makazi ya wakimbizi.

Aidha, kwa Tangazo la Serikali Na. 600 la tarehe 03 Oktoba, 2025, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alitoa Amri ya Marekebisho ya Amri ya Mgawanyo wa Maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya Mwaka 2025 kwa kuzifuta kata kumi (10) za Litapunga, Kanoge, Katumba na vijiji viwili (02) vya Ikolongo na Ndurumo vya Kata ya Mtapenda Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mkoa wa Katavi.

Kata nyingine ni Mishamo, Ilangu, Bulamata na Ipwaga zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi na kata za Milambo, Igombemkulu na Kanindo zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua Mkoa wa Tabora.

*Ndugu Wananchi,*

Kwa kuwa, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, amezifuta kata tajwa, na

Kwa kuwa masharti ya kifungu cha 5(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 yanaitaka Tume kutumia kata zilizoanzishwa na



UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura

Waziri Mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuwa kata kwa madhumuni ya uchaguzi wa madiwani; na

Kwa kuwa kanuni ya 4 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 inatoa mamlaka kwa Tume kufanya mabadiliko ya mipaka ya maeneo ya uchaguzi pale yanapotokea mazingira yatakayoathiri mipaka iliyopo ya maeneo ya uchaguzi ikiwemo kufutwa kwa kata au kijiji; na

Kwa kuwa Tume iliwateua wagombea Udiwani saba katika kata saba ambazo ni miongoni mwa kata kumi (10) zilizofutwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 26 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025; na

Kwa kuwa kufutwa kwa kata husika kunaziondoa kuwa eneo la uchaguzi,

Hivyo, Tume katika kikao chake kilichofanyika tarehe 06 Oktoba, 2025 na kupitia Tangazo la Serikali Na. 604 la tarehe 10 Oktoba, 2025 imefanya uamuzi ufuatao:

1. Kuzifuta kata kumi (10) zilizofutwa na Waziri Mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kutoka katika maeneo ya uchaguzi wa madiwani kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; na
2. Kutengua uteuzi na kuwaondoa katika orodha ya wagombea udiwani saba (07) walioteuliwa katika kata husika. Wagombea waliotenguliwa uteuzi wao na kuondolewa kwenye orodha ya wagombea ni hawa wafuatao:

| Na. | Jina la Mgombea | Kata aliyokuwa ameteuliwa kugombea | Chama cha Siasa |
|---|---|---|---|
| 1. | Salehe Mrisho Msompola | Kanoge | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 2. | Elius Wilson Elia | Katumba | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 3. | Mohamed Ally Asenga | Litapunga | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 4. | Nicas Athanas Nibengo | Bulamata | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 5. | Sadick Augostino Mathew | Ilangu | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 6. | Rehani Simba Sokota | Ipwaga | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 7. | Juma Mohamed Kansimba | Mishamo | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |



UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura

Kata tatu zilizofutwa za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Mkaoni Tabora hazikufanya uteuzi wa wagombea wa Udiwani, kata hizo ni Milambo, Igombemkulu na Kanindo.

*Ndugu wananchi,*

Kutokana na mabadiliko hayo, Tume imevifuta vituo 292 vya kupigia kura vilivyokuwa kwenye kata zilizofutwa na kwa kushauriana na watendaji wa uchaguzi wa maeneo husika na kwa kuzingatia ukaribu wa maeneo wanayoweza kufika wapiga kura, Tume imeanzisha vituo 292 vya kupigia kura katika maeneo jirani na kata zilizofutwa ili kuwawezesha wapiga kura kutoka maeneo yaliyofutwa kwenda kupiga kura.

*Ndugu Wananchi,*

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 19(3)(c) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, wapiga kura 106,288 waliokuwa kwenye vituo vilivyofutwa wamehamishiwa kwenye vituo 292 vya kupigia kura vilivyoanzishwa katika kata za Mtapenda, Uruwira, Nsimbo na Ugala zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mkoa wa Katavi. Kata nyingine walizohamishiwa ni Sasu, Ilege, Uyowa, Makingi na Silambo zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua Mkoa wa Tabora na Kata ya Tongwe iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi.

*Ndugu wananchi,*

Tume inatoa wito kwa wananchi kuzingatia mabadiliko haya ya maeneo ya uchaguzi ili waweze kutumia haki yao ya msingi ya kushiriki kupiga kura siku ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani tarehe 29 Oktoba, 2025.

**"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"**

Imetolewa leo tarehe 12 Oktoba, 2025; na

Jaji (Rufaa) Jacobs C.M. Mwambegele

**MWENYEKITI**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**



UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura